

2. مَدُّ الْبَدَل Maddul-Badal

Kanuni ya badal: ni kuja kwa hamzah mbili zenye kufuatana moja baada ya nyengine, ya kwanza ikawa na *i'raab* na ya pili ikawa saakin katika neno moja, hivyo hubadilishwa hamzah ya pili saakinah na kuwa herufi ya madd yenye kuwiana na *i'raab* ya hamzah ya kwanza.

Hukmu yake ni kuvutwa harakah mbili.¹

Mfano jina la Aadam asili yake ni **ءَأَدَمَ** (A-dam); Hamzah mbili zenye kufuatana moja baada ya nyengine, ya kwanza ina *i'raab* ya fat-hah na ya pili ina sukuwn. Hamzah ya pili saakinah imebadilishwa na kuwa herufi ya madd yenye kuwiana na *i'raab* ya hamzah ya kwanza hivyo kusomwa: **آَدَمَ**.

Mifano ifuatayo yote asili ya herufi ya madd katika mifano hii ni hamzah imebadilishwa na kuwa herufi ya madd yenye kuwiana na *i'raab* ya hamzah ya kwanza:

Mwanzo wa neno

ءَأَمِنُوا إِيمَنَّا وَأَوْذُوا

Katikati ya neno

الْقُرَّانَ مُتَّكِينٍ يَعُودُهُ

Mwisho wa neno

رءَا وَبَاءُوا ءَأَبَاءِي

¹ Hafsw 'an 'Aaswim *twariyq Ash-Shaatwibiyyah* huivuta harakah mbili. Ama riwaayah nyinginezo huvutwa zaidi ya harakah mbili, ndio maana Maulamaa wa fani hii wakaona kwamba hukmu hii ya مَدُّ الْبَدَل (maddul-badl) ihusiane na mlango huu wa مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) badala ya mlango wa مَدُّ الْفَرْعِي (maddul-far-'iy)